East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687
EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# TAMATHALI ZA SEMI ZINAZOSAWIRI UBABEDUME KATIKA MAJIGAMBO YA MIVIGA YA *SHILEMBE* NA MCHEZASILI WA *MAYO* YA WAISUKHA, NCHINI KENYA KWA MTAZAMO WA SEMANTIKI

*Mary Lukamika Kibigo[1], Dr. Susan Chebet Choge[2] & Dr. Fred Wanjala Simiyu[3]*

[1]Masinde Muliro Univesrty of Science & Technology, P. O. Box 190 – 50100, Kakamega, Kenya, kibigomary@gmail.com.
[2]Masinde Muliro Univesrty of Science & Technology, P. O. Box 190 – 50100, Kakamega, Kenya, schoge@mmust.ac.ke.
[3]Kibabii University, P. O. Box 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, wsimiyu@kibu.ac.ke.

**Article history:**

*Received: 29 Aug 2019*
*Accepted: 03 Sep 2019*
*Published: 06 Sep 2019*

**Keywords**:

*Ubabedume,*
*Upiganishaji Fahali,*
*Majigambo,*
*Shilembe,*
*Mayo*

## IKISIRI

Makala hii imewasilisha baadhi ya matokeo ya utafiti wa Uzamifu uliotafitia ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *mchezasili* wa *Mayo* katika jamii ya Waisukha nchini Kenya kwa mtazamo wa semantiki. Utafiti huu ulihakiki tamathali mbalimbali za semi ambazo ni chuku, jazanda na majazi miongoni mwa nyingine kwa kutumia mtazamo wa kisemantiki ili kudhihirisha namna zinavyosawiri ubabedume katika miviga ya *Shilembe* na Mchezasili wa *Mayo.* Utafiti huu ulifanyika katika Kaunti Ndogo ya Shinyalu, Kaunti ya Kakamega, nchini Kenya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili, ya kwanza ni nadharia ya Uwezo-Uume iliyoasisiwa na Robert Bly na kuendelezwa na Izugbara. Inahusu mahusiano ya wanaume na wanawake katika jamii. Nadharia ya pili iliyotumiwa ni ile ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (UCHAMAWADI). Nadharia hii ina misingi yake katika kazi mbalimbali za wataalam tofauti ulimwenguni. Nadharia mbili zilitumiwa ili kuoanisha taaluma ya Fasihi na Isimu. Utafiti huu ulitumia majigambo kumi na sita kwa kutumia uchunzaji-shiriki, dodoso, unasaji sauti na ujazaji wa hojaji. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa lugha ya majigambo inayoghaniwa na fanani hubeba tamathali za semi zinazosawiri ubabedume. Hivyo, sherehe hizi zitumiwe kama jukwaa la kuelimisha vizazi vichanga vya jamii hii kuhusu mila na desturi zao. Utafiti huu umeonyesha kuwa Fasihi Simulizi ya Mwafrika ni hai. Utafiti umegundua kuwa, lugha ni kipengele muhimu katika jamii. Hata hivyo, utafiti umetambua kuwa, wakati mwingine lugha hutumiwa vibaya na wanajamii kumtukuza Mwanamume kupita kiasi na kumpa uwezo na mamlaka dhidi ya mwanamke. Isitoshe, ubabedume umejengwa katika mila, itikadi na utamaduni wa jamii husika. Makala hii imeweka wazi baadhi ya matokeo ya utafiti huu.

## UTANGULIZI

Huwezi kushughulikia dhana za *Shilembe* na *Mayo* katika jamii ya Waisukha bila kuzihusisha na upiganishaji fahali. Dhana ya kupiganisha fahali ina historia ndefu na mkufu huu tunaweza kuufuatilia kuanzia kule Mesopotamia ambapo fahali waliabudiwa na kutolewa kama sadaka kwa

miungu. Upiganishaji fahali ulihusishwa na Wagiriki pamoja na visaviini na visakale vyao. Katika karne ya kumi na tisa kule Ufaransa, wanajamii walianzisha upiganishaji fahali kwa njia yao ya kipekee. Michezo hii ilienea na kuwa katika mabara ya Uropa, Asia na Afrika. Nchini Tanzania, mchezo huu uliasisiwa na Wareno katika visiwa vya Pemba na Unguja na ulijulikana kama *mchezo wa ng'ombe*. Magharibi mwa Kenya, fahali hupigana na fahali mwingine kwa kutumia pembe. Wanyore huiita sherehe hii *Eshilembe*, nao Wamaragoli huiita *Ekeremba* ilhali Waisukha huiita *Shilembe*. Miviga ya *Shilembe* hufanywa tu kaburini mwa Mwanamume Mwisukha aliyepata ushujaa kwa kumuua adui wao kama vile Wazungu waliowatawala na Wanandi waliowaiba ng'ombe wao. Sherehe hii huhusisha upiganishaji wa fahali kaburini mwake siku moja baada ya mazishi. Kutokana na athari za kidini na usasa, si rahisi kufanywa kwa sherehe hii katika enzi hizi, hata hivyo kuna nasaba za Waisukha ambazo zingali zinashikilia itikadi hii. Nayo *Mayo* ni miviga ya *Shilembe* ambayo imebadilishwa na kuwa mchezo wa kiasili wa Waisukha. Jinsi ilivyo katika *Shilembe, Mayo* pia huhusisha upiganishaji wa fahali na mara nyingi huchezwa wakati wa siku kuu za kitaifa ama za kijamii kama maonyesho ya sanaa na kwa ajili ya mashindano au burudani. Vilevile, sherehe za *Mayo* hufanywa siku za Jumamosi na huhusisha upigaji wa ngoma za Isukuti na kupiganisha fahali. Katika sherehe hizi mbili za *Shilembe* na *Mayo*, majigambo hughaniwa na fanani watambaji (Hemingway, 1932; Alembi, 2002; Kabaji, 2005 & 2008; Kibigo, 2019).

## NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti wa makala hii umeongozwa na nadharia mbili za Uwezo-Uume na UCHAMAWADI. Wanjala (2011 & 2015) anaeleza kuwa nadharia mbili au zaidi zinaweza kutumiwa kutegemea na malengo ya utafiti husika. Hivyo basi, lengo kuu la kuzitumia nadharia hizi katika makala hii lilikuwa ni kuoanisha taaluma ya Fasihi Simulizi kwa kujikita katika majigambo na taaluma ya Kiisimu kwa kushughulikia uhakiki wa tamathali za semi Kisemantiki.

### Nadharia ya Uwezo-Uume

Nadharia hii inahusisha dhana mbili; **Uwezo** na **Uume**. Inarejelea uwezo ambao jamii mbalimbali huwapa wanaume. Nadharia hii iliasisiwa na Robert Bly (Wells & Holland, 2001) na kuendelezwa na Izugbara mnamo mwaka wa 2005 (Izugbara, 2005). Kwa mujibu wa Kibigo (2019), nadharia hii hubainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume, hasa kutokana na utamaduni wa jamii husika. Dhana 'mwanaume' ipo katika misingi ya kibiolojia ilhali 'ubabedume' au 'uanaume' hutokana na mielekeo, imani na matarajio ya utamaduni wa jamii husika. Mtaalam huyu anaeleza kuwa ubabedume huzaliwa na kukuzwa na utamaduni na pia huhalalishwa kwa njia, hali na nyakati tofauti za jamii husika. Nadharia hii hufungamanishwa na *dhakari* na wenye kuimiliki hujamiishwa kama rasilmali yenye manufaa makubwa kwa jamii. Hii ndiyo sababu ambayo huifanya jamii kumchukulia mwanamume kwa njia chanya na kumchukulia mwanamke kwa njia hasi. Mwanamume huchorwa akiwa na sifa kama vile, uwezo, uvumilivu, ushujaa na ujasiri. Kwa upande mwingine, mwanamke husawiriwa akiwa na sifa kama za uoga, kutothubutu mambo na kadhalika. Kwa hivyo, sura ya wanaume hujengwa kutokana na matarajio ya kiitikadi na kitamaduni kuwahusu. Izugbara (2005, p. 13) katika kusisitiza umuhimu wa dhakari katika kuipa jinsia ya kiume mamlaka zaidi anasema:

> *[…] umbo la dhakari…na uwezo wake kuwa ngumu, kubwa, thabiti na yenye nguvu wakati wa mchechemo ni dhihirisho […] kuwa dhakari ina uwezo! shahawa ambayo inaitoa katika kipindi cha tendo la ngono huonekana kama sumu ambayo humdhoofisha mwanamke, […] matokeo muhimu huhusishwa na amali ya dhakari na upenyezi wake katika kuupoteza ubikira na kutia mimba mwanamke, […] hali hii imeipa dhakari umuhimu ambao umeitawaza juu ya uhai na ufu […]*

Mihimili ya nadharia hii ni kama ifuatayo:

i. Itikadi za kijamii huongoza fikra kwamba, utawala wa mwanamume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulisho vya jinsia ya

kiume maandishi, matukio na maelezo ya kihistoria kwa misingi ya jamii husika (Wells & Holland, 2001).

ii. Utamaduni, lugha, imani na desturi zimewawezesha wanaume kuwa watawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilmali zenye thamani katika jamii kama vile, shamba, kazi, pesa na taasisi za kijamii zenye nguvu kama vile serikali na dini (Collins, 1971; Sokoloff, 1980).

iii. Majukumu yanapogawanywa kiuana, wanaume huweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu wa kiume kwa manufaa yao, wakisisitiza kwamba, 'Mungu wa kiume' alimpa mwanamume mwanamke kama mwenzi wake (Ruether, 1974).

iv. Sifa angama za uume na maeneo ya ubabedume yanayojitokeza katika desturi kwa jumla kupitia: maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi na kukidhia familia, kuwa na tajriba na shari ya kijinsia, ukakamavu, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani na kuthubutu mambo (Chafetz, 1974; Doyle, 1985).

Teneti hizi zimejikita katika utamaduni, itikadi za jamii, mgawanyo wa mamlaka na uwezo wa kijinsia, mielekeo na matarajio ya jamii kumhusu kila mwanajamii. Makala hii imetumia mihimili mitatu – i, ii & iv. Nadharia hii ilikuwa mwafaka kwa vile majigambo ya miviga ya *Shilembe* na mchezasili wa *Mayo* husheheni taasubi za kiume zinazodhihirika kupitia tamathali mbalimbali za usemi zilizotumiwa.

**Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (UCHAMAWADI)**

Nadharia ya pili iliyotumika katika utafiti wa makala hii ni ile ya **U**changanuzi **Ma**kinifu **wa Di**skosi (UCHAMAWADI) iliyoasisiwa katika miaka ya 1990 na Teun Van Dijk, Norman Fairclough, Gunther Kress, Theo van Leeuwen na Ruth Wodak (Kibigo, 2019; Choge, 2018; Wodak, 2013; Wodak & Meyer, 2008; Fairlough, 2002; Van Dijk, 2000). Katika makala hii nadharia hii imerejelewa kwa akronimu UCHAMAWADI iliyoibuliwa na kutumiwa na Choge (2018). Choge anaeleza kuwa mhakiki yeyote yule hana budi kuyachanganua matini kwa umakini na uangalifu ili aweze kupata matokeo mwafaka kisayansi. Msingi wa nadharia hii ni kazi za wataalamu mbalimbali katika sanaa ya unenaji, isimu matumizi, isimu jamii, isimu matini na isimu amali. Dhana za itikadi, uwezo, mgawanyo msonge wa majukumu na uana huchukuliwa kama vibadiliki vya msingi katika ufafanuzi wa matini. Nadharia hii ilikuwa nanga muhimu kwa utafiti huu kwa vile ilimwezesha mtafiti kuyachanganua majigambo teule ya makala hii.

**Tamathali za Semi zinazosawiri ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mayo***

Makala hii inawasilisha matokeo ya utafiti ya udhihirisho wa ubabedume katika majigambo ya *miviga ya* S*hilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* miongoni mwa Waisukha wanaoselelea katika Kaunti Ndogo ya Shinyalu, Kaunti ya Kakamega nchini Kenya. Ubabedume umedhihirishwa kupitia tamathali za semi kama vile chuku, jazanda na majazi. Uchunguzi wa tamathali hizo za usemi ulichochewa na utata wa dhana hiyo. Wataalam wengi wameweza kuchangia kwa kutoa fasili anuwai. Dhana hiyo inajulikana kama tamathali za usemi kama anavyodai Simala (2013). Anaeleza tamathali za usemi kama maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na msanii ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi au kusema. Dhana hii iliusaidia utafiti huu kuzua hali ya mwingiliano taaluma kwa vile kuna vipengele kadhaa katika maelezo ya Simala vinavyohusu taaluma ya Isimu na vilevile taaluma ya Fasihi. Kwa mfano, katika maelezo yake kuna dhana ya sauti inayojikita katika taaluma ya Kifonetiki na Kifonolojia. Kuna dhana ya nomino inayorejelea taaluma ya Kimofolojia, vishazi inayoashiria taaluma ya Kisintaksia na maana inayorejelea taaluma ya Semantiki. Mtindo nao hurejelea mbinu inayotumiwa na msanii ili kudhihirisha upekee wa kazi yake. Hali hii ndiyo iliyousaidia utafiti huu kutambua kipengele cha kiisimu, Semantiki kilichousaidia utafiti huu kuzihakiki tamathali za semi.

Kwa upande mwingine, tamathali za usemi hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya Fasihi na kuongeza utamu wa lugha (Senkoro, 1985; Gafkosoft, 2017). Mawazo ya wataalam hawa

yanasisitiza dhima ya tamathali ya kuwasilisha maana, mtindo na kuipamba lugha. Hata hivyo, ingawa neno tamathali lina asili yake katika neno mithilisha lenye maana ya kufananisha, ni muhimu kufahamu kuwa tamathali za usemi hufanya kazi ya kufananisha dhana moja kwa nyingine tofauti. Aghalabu hutumiwa kurejelea usemi ubadilishao maana dhahiri au za kawaida za maneno kuleta maana maalum ya fasihi iliyokusudiwa na msanii. Wataalam hawa wanakubaliana kwamba ni fungu la maneno lililogeuzwa maaana yake ili kuwakilisha maana nyingine. Kwa hivyo, katika tamathali za usemi kuna maana na matumizi mengine ya kisanii (Msokile, 1992; Mwamanda, 2008).

Janovsky (2014) anahoji kuwa tamathali za usemi kwa ujumla ni hali ya kuzungumzia jambo kwa kumaanisha jingine. Katika kazi hii, tamathali za usemi zimetumika kurejelea kipengele cha kiisimu ambacho ni semantiki na nafasi yake katika kuzihakiki tamathali za usemi.

**Majazi na Semantiki**

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2015) inasema kuwa majazi ni jina analopewa mtu ambalo hufanana na tabia au umbile lake kwa mfano Cheupe, Kidevu na Majivuno. Mwita (2005) anaeleza kuwa dhana ya majazi inarejelea mbinu wanayotumia wasanii wa kazi za kifasihi ili kumpa mhusika jina linalolingana na sifa, matendo au hulka zake. Naye Wafula (1999) anafafanua kuwa majazi ni mbinu kongwe, aghalabu inapotumiwa na wanafasihi huwa imenuiwa kuoanisha majina ya wahusika au mahali na dhana, hisia au tajriba zinazowasilishwa na kukisiwa katika majina hayo. Wamitila (2003) anasema majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi au yanayotuelekeza kwenye wasifu wa tabia zao. Kutokana na fasili za wataalam hawa, hadhira huweza kubaini tabia ya mhusika au fanani na nafasi yake katika kuweka wazi lengo la jigambo lake.

Katika majigambo ya Waisukha, fanani hutumia vipashio mbalimbali vya lugha kufumbata majazi yanayolenga katika kujenga, kuendeleza na kudumisha picha mbalimbali za ubabedume kutegemea mjigambi husika. Mawazo ya Simala (2012) yanaonyesha utata katika dhana ya mafumbo ambayo huwa na istilahi nyingi kama vile tashbihi, uhaishi na jazanda. Anahoji kuwa, hizi ni tamathali za usemi zinazohusiana na maana za kauli. Katika msingi huu, cha kigezo cha maana pia huweza kudhihirika katika majazi. Anavyodai Matinde (2012), semantiki ni taaluma inayojikita katika ufasiri wa maana katika kiwango cha sentensi kwa kuchunguza miundo mbalimbali kwa mfano anomali, ukinzani, itkisadi na utata miongoni mwa miundo mingine. Katika majigambo ya Waisukha, hali hii pia ilidhihirika katika baadhi ya majigambo. Tazama jigambo la kwanza, ubeti wa pili:

**JG 1 Jigambo la 1** (Taz. Jigambo la 6 katika Kibigo, 2019, p. 148 ubeti wa pili)

| ***Kiisukha*** | ***Tafsiri katika Kiswahili*** |
|---|---|
| 1. *Inzi ni muyayi wa tata* | Mimi ni mvulana wa baba |
| *Wavaya tsichilishi tsinyishi* | Aliyewafuga fahali wengi |
| *Tsiamela tsinziga* | Wameota pembe |
| *Tsiasinjila vulahi* | Zilizosimika vizuri |
| *Bahilana ni bibula bana banyishi* | Wakaoana na kuzaa watoto wengi |
| *Ni bilachi ya malova* | Wengine ni wa kikahawia |
| *Indavu nende imwamu, manya isekese* | na meusi mfano wa tausi |
| | |
| 2. *Tata ni mubayi witsichilishi tsiakhomela* | Baba ni mfugaji wa fahali wanene |
| *Sindateshia tawe habula omwana wanje* | Sijaoa ila mwanangu |
| *Alangungwa Spana* | Anaitwa Spana |
| *Utechilitsanga shibala shiosi shi* | Anayetetemesha nchi yote |
| *Tsimbia tsiosi tsi Isukha* | Na koo zote za Waisukha. |
| *Bakhali vosi bamuyanza* | Wanawake wote wanampenda |
| **(Ukokotozi Nyanjani)** | **(Tafsiri: Watafiti)** |

**Tashbihi na Semantiki**

TUKI (2004) wanaeleza tashbihi kama msemo wa kulinganisha ambayo hufananisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno: kama, ja, mfano wa, kana kwamba au mithili ya. Mwita (2005) akikubaliana na hoja hii anahoji kwamba tashbihi ni maneno yanayofananisha jambo, kitu, hali au kitendo na kingine kwa kutumia vihusishi kama vile, kama, mfano wa, ja, mithili ya na mengine mengi. Mawazo ya wataalam hawa yanakaribiana na Kimani na Chimera (1999) wanaodhukuru kuwa tashbihi ni maneno yanayofananishwa (au kushabihisha) kitu, jambo au kitendo na kingine kwa kutumia vihusishi kama vile kama, ja, mithili ya, mfano wa na kadhalika. Hivyo, fasili za wataalam hawa zinafumbatwa na Arege (2002) anayesema kuwa:

Tashbihi ni dhana ambayo inatumiwa katika kurejelea hali yoyote ile ya ulinganishi wa watu au vitu na watu au vitu vingine kwa kutumia maneno ya kuungia kama vile, mithili ya, mfano wa, kana kwamba, ja, sawa na miongoni mwa mengine. (TY).

Kauli za wataalam hawa ni muhimu kwa vile zinarejelea ile hali ya kufananishwa kwa vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno ya kulinganisha. Hii ni mbinu inayotumiwa katika kulinganisha kwa kuchora picha au taswira halisi kuhusu kusudi la msanii. Anayejigamba hujifananisha na vitu au hali nyingi na wala si wanyama tu. Anaweza kujifananisha na aila yake, wazazi wake, mashujaa fulani katika jamii, waasisi wa jamii yake, miamba, moto na vitu vingine vilivyo hatari katika ulimwengu kijumla. Msanii hutumia vipashio mbalimbali vya lugha vinavyosheheni tashbihi na ambavyo hujenga ubabedume. Mifano ifuatayo inaonyesha jinsi fanani mjigambi anavyotumia kipashio hicho cha lugha katika kukuza na kudumisha ubabe na taswira za kiuwezo kwenye majigambo ya Waisukha wanapopiganisha fahali. (Taz. jigambo la 8, mshororo wa nne katika Kibigo, 2019). Fanani mjigambi anasema, ‘Mwenye nguvu kama simba’ kurejelea fahali wa ukoo wa Avateheli ambao hawashindwi kamwe vitani hususan wanapopiganisha fahali. Tashbihi hii inarejelea ukali wa mwanamume ambaye akiwa katika boma hakuna anayethubutu kuleta mchezo au kufanya mambo ya kiupuzi, awe ni bibi au mkewe, watoto na hata majirani. Ukali wa simba umetumiwa kama kiarifu kidokezi cha nguvu na uwezo alio nao mwanamume bila kuhitaji msaada wowote. Isimu maana ama semantiki huchunguza maana katika lugha ya binadamu (Habwe & Karanja, 2004).

Katika hali hii, ni bora kutambua kuwa Majigambo ya Waisukha yalijikita katika kuweka wazi matumizi ya tashbihi na vilevile matumizi ya kiwango cha Kiisimu cha Semantiki ili kudhihirisha na kusawiri ubabedume. Katika kuangazia kiwango cha Kisemantiki, (tazama mshororo wa kwanza katika jigambo la 16 kwenye kiambatisho B katika Kibigo, 2019) Fanani mjigambi hutumia tashbihi kujilinganisha na ushujaa fulani. Katika majigambo, tashbihi aghalabu hutumiwa katika ulinganishi wa watu, wanyama, hirimu, hali, ukoo au nasaba na vitu vingine mbalimbali ili kuonyesha sifa za kiubabe. Kwa upande mmoja, mwanamke huweza kupewa sifa zilizo duni au zilizodhalilishwa na kumlinganisha na wanyama waoga kama vile kunguru ilhali mwanamume hulimbikiziwa sifa za kumjenga kama mwenye uwezo, maamuzi, mamlaka, shujaa na huweza kulinganishwa na wanyama hatari, hali ngumu na vitu mbalimbali na vyenye nguvu katika jamii kama vile, moto, radi, mwamba, ngwena, chatu na kadhalika. Hivyo, mwanamke huonekana kama jinsia tegemezi ambayo, kulingana na mila, itikadi, desturi na utamaduni wa Waisukha, wako chini ya mamlaka ya jinsia ya kiume. Hebu rejelea majigambo ya 8, 9 na 16 katika Kibigo (2019) yanavyozua ubabedume kitashbihi kwa mtazamo wa kisemantiki:

**JG 2 Jigambo la 2** (Taz. Jigambo la 8 katika Kibigo, 2019, p. 148)

| *Kiisukha* | *Tafsiri katika Kiswahili* |
|---|---|
| *Luyia lwa Bateheli* | Wa ukoo wa Avateheli |
| *Khali nameneshe angwetsanga* | Hata akivunjika huungwa |
| *Khuvumishi masamba kishimwa* | Kwa kutumia dawa ya kienyeji |

| | |
|---|---|
| *Mwene tsingulu khuli isimba* | Mwenye nguvu kama simba |
| *Hurenjitsanga shibara shioshi* | Anayetetemesha dunia nzima |
| *Khuli shivala shia shikuri shitsi ndege* | Kwenye eneo kame la uwanja ndege |
| *Khuli shiahionilwa vulavu* | Kama kwamba linachochewa nuru |
| **Chanzo: Ukokotezi Nyanjani** | **(Tafsiri: Watafiti)** |

**JG3 Jigambo la 3** (Taz. Jigambo la 9 katika Kibigo, 2019, p. 149)

| ***Kiisukha*** | ***Tafsiri katika Kiswahili*** |
|---|---|
| *Nachenda Isukha yiosi* | Nimetembea Isukha kote |
| Nise Eminyi-linyoni | Mimi ndiye Eminyi-ndege |
| *Nakona khali uwanja ndege* | Nikalala hata Kiwanja Ndege |
| *Havakwanyinga tsichilishi* | Wanaopiganisha fahali |
| *Bakhanga khuli mulilu* | Wamewaka kama moto |
| *Mulili mwichenda nyama* | Moto wa jangwani |
| *Babimanga bura* | Wanalenga mishale |
| *bura bwi sumu* | Mshale ukiwa na sumu |
| *Khumanyinya buhaka bwabwo* | Ili kuonyesha ushujaa wao |
| *Nibalwaninyanga tsichilishi* | Wanapopiganisha fahali |
| **Chanzo: Ukokotezi Nyanjani** | **(Tafsiri: Watafiti)** |

**JG 4 Jigambo la 4 (Taz. Jigambo la 16 katika Kibigo 2019 p, 153)**

| ***Kiisukha*** | ***Tafsiri katika Kiswahili*** |
|---|---|
| 1.*Omuhaka nitsi wonyene* | Shujaa ni mimi tu |
| *Mwene tsingulu khuli isimba* | Mwenye nguvu kama simba |
| *Nitsi owamanya okhulwanya itsichirishi* | Mimi ninajua kupiganisha fahali |
| *Sinjendananga vutswa tawe* | Sitembeitembei tu ovyo |
| *Khandi mbula bulalu* | Tena sina kichaa |
| | |
| 2. *Inzi nwaaninja* | Mimi ninapiganisha |
| *Tsichirichi khuli* | Fahali kama ambaye |
| *Manya sinanwaninje* | Sitafanya hivyo |
| *Kho khandi* | Tena |
| **Chanzo: Ukokotezi Nyanjani** | **(Tafsiri: Watafiti)** |

### Chuku na Semantiki

Dhana ya chuku imefasiliwa na Kimani na Chimera (1999) kama hali ya kutia chumvi kwa minajili ya kuathiri hisia. Wanaeleza kuwa chuku hudokeza hali ambayo inakiuka mipaka ya kiuhalisia. Tamathali hii imetumika na semantiki katika utafiti huu kuonyesha kuwa inajengwa na vipashio vya lugha ambavyo kwa namna ya kipekee hutumiwa na msanii kuijenga picha aliyoikusudia yeye mwenyewe. Katika majigambo ya Waisukha kuna upigaji chuku ambao mjigambi anatumia ili kujenga na kukuza sifa za ubabedume. Kwa mfano, katika jigambo la 11 mshororo wa 6 (Rej. katika Kibigo,2019), kuna upigaji chuku kwa vile msanii anasema kuwa ‘fahali wa ukoo wa Avisende wanajua kufanya ili wanawake wapate mimba.’ Msanii ametumia sifa ya kujua kufanya kama kidokezi muhimu cha ubabedume unaojengwa na utendaji wa umbile la kiume kisemantiki. Rejelea jigambo la tano (JG 5) lifuatalo.

**JG 5 Jigambo la 5** (Taz. Jigambo la 11 katika Kibigo, 2019, p. 150)

| ***Kiiisukha*** | ***Tafsiri katika Kiswahili*** |
| --- | --- |
| *Nuwisunda himbi handi* | Ukisogea karibu nami |
| *Kenyanga wekasie ubulahi* | Ni sharti ujihami vilivyo |
| *Habula ndio alanyakhana* | La sivyo atajutia laitani |
| *Rulanga mumuliango kwa Abisende* | Mimi ni wa ukoo wa Avisende |
| *Mwene itsichirishi tsyobucheli* | Mwenye fahali walio na hekima |
| *Vamanya khukhola avakhali vanyole tsinda* | Wanajua kufanya wake wapate mimba |
| *Avasiani avarambi tsifuti tisa* | Wavulana warefu futi tisa |
| **Chanzo: Ukokotezi Nyanjani** | **(Tafsiri: Watafiti)** |

Upigaji chuku pia umejitokeza katika jigambo hili la kumi na moja katika mshororo wa mwisho unaosema 'wavulana warefu futi tisa'. Fanani mjigambi ameitumia sifa ya urefu wa mwanamume kuashiria dhana ya ubabedume unaojengwa na maumbile ya wanaume. Wanaume wa ukoo wa Abisende wanaaminika kuimiliki sifa hii ya urefu wa futi tisa ambao ni urefu unaoweza kukatwa mara mbili na kuumba watu wengine wawili. Hali hii inazua ubabedume kwa misingi kuwa urefu wa mwanamume huangazwa kwa njia chanya ilhali ufupi wa mwanamume huangazwa kwa njia hasi. Hata hivyo, kuna baadhi ya fanani watambaji wanaodokeza kuwa urefu au ufupi wa mwanaume haujalishi, lililo muhimu ni sifa za ubabe.

Katika ubeti huu, fanani mjigambi anapiga chuku kwa kutudokezea kuhusu kumiliki fahali wenye hekima ambao ni wanaume wanaojua kutafuta mali katika jamii. Wanaume ndio wanarejelewa kuwa wenye akili katika jamii hii. Kwa hivyo, wao ndio wana akili ya kuweza kumiliki mali dhidi ya wanawake na hata kuweza kuitunza mali hiyo.

**Jazanda na Semantiki**

Mwita (2005) anasema kuwa jazanda ni maneno yanayotumika kugubika ujumbe fulani. Msikilizaji au msomaji hana budi kulifumbua fumbo hilo iwapo atapata ujumbe unaodhamiriwa. Kimani na Chimera (1999) nao wanahoji kuwa jazanda ni mafumbo ambayo ndanimwe maana ya kitu imefichama. Ni sawa na istiara, yaani, kilichosetiriwa. Naye Wamitila (2003) anaihusisha jazanda na taswira. Mawazo ya wataalam hawa yalikuwa msingi bora katika utafiti huu. Katika mantiki hii, tukirejelea majigambo ya Waisukha, wasanii wengi hutumia jazanda hususan katika kuibua taswira mbalimbali zinazoonesha ubabedume. Jazanda hizi hutumiwa kisemantiki katika usimbaji na matumizi ya baadhi ya maneno ambayo yanatumika katika kurejelea falsafa, mitazamo, mielekeo, matarajio na thamani za kijamii kuhusu sifa mbalimbali za ubabedume. Rejelea jigambo la sita lifuatalo:

**JG 6 Jigambo la 6** (Taz. Jigambo la 14 katika Kibigo, 2019, p. 150)

| ***Kiisukha*** | ***Tafsiri katika Kiswahili*** |
| --- | --- |
| *Nitse mwiroli wamanyikhana* | Mimi ni mjigambi hodari |
| *Owamanya okhulwanyanga itsichirishi* | Ninayejua kupiganisha fahali |
| *Ndayanzwa ni tsingombe tsinyingi* | Ninapendwa na ng'ombe wengi |
| *Tsisievitsanga visindi* | Wanaotingisha viuno |
| *Khurula muluyia lwa Vayokha* | Kutoka ukoo wa Vayokha |
| *Ndahura vandi voosi* | Ninawashinda wengine wote |
| *Mbetsaanga imberi vuri lwosi* | Niko mbele kila mara |
| *Ndahura khuri itai* | Kama tai |
| *Vandi vali inyima khuri likoti* | Wengine wako nyuma kama koti |
| **Chanzo: Ukokotezi Nyanjani** | **(Tafsiri: Watafiti)** |

Katika jigambo hili, jazanda imejitokeza katika kauli hii 'mimi ni fahali hodari ninayependwa na ng'ombe wengi'. Jazanda hii inaashiria ukware kama sifa kuu ya ubabedume. Hii ina maana kwamba wanaume ndio wana uwezo wa kuoa wanawake wengi katika jamii kinyume na wanawake.

**Methali na Semantiki**

Arege (2002) katika Matinde (2015) anaeleza kuwa methali ni fungu la maneno yaliyotumiwa pamoja kisanii yenye maana ambayo ni ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa. Methali huwa na dhima mbalimbali katika jamii, kwa mfano huweza kutoa maadili, kukejeli, kukaripia na kupitisha hekima mbali na kusawiri na kuyakinisha mandhari ya kitamaduni ya jamii inayozitunga na kuzitumia.

Katika makala hii, methali zimetumika katika majigambo ili kubainisha itikadi za kiubabe. Mathalan katika jigambo la saba, 'Fahali ni moto wa koko, usipowaka utafuka'. Methali hii katika Kiswahili huwa hivi: Mume ni moto wa koko, usipowaka utafuka. Katika utafiti huu, methali hii inarejelea sifa za mwanaume au hata kuzisambaza mbegu zake mahali pengi, yaani kuzaa watoto wengi na wanawake tofauti. Rejelea jigambo la saba lifuatalo:

**JG 7 Jigambo 7** (Taz. Jigambo la 2 katika Kibigo. 2019, p. 146)

| ***Kiisukha*** | ***Tafsiri katika Kiswahili*** |
|---|---|
| *Bisukha oyee!* | Waisukha oyee |
| *Nitsi itaywa* | Ni mimi jogoo |
| *Bisukha yaa!* | Waisukha yaa |
| *Mbulili mnanganga* | Nimesikia mmeniita |
| *Muliango kwa mundu hu moyo mulayi* | Mlango wa mwenye moyo safi |
| Ichirishi no muliro mukali | Fahali ni moto wa koko |
| Nikulahamba kulatuma | Usipowaka utafuka |
| *Mulwani hatari hukhabaila* | Mpiganaji hodari msimchezee |
| **Chanzo: Ukokotezi Nyanjani** | (**Tafsiri: Watafiti)** |

Jedwali 1 lifuatao ni muhtasari wa tamathali za usemi zinazodhihirisha ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na mchezasili wa *Mayo* zilizochamuliwa katika makala hii (Kibigo, 2019. p, 148-153).

**Jedwali 1 Tamathali za Usemi zinazosawiri Ubabedume katika Majigambo**

| Jigambo | Tamathali za Usemi | Mfano | Ubabedume |
|---|---|---|---|
| 7 | Methali | Fahali ni moto wa koko usipowaka utafuka | Sifa za mwanamume kusambaza mbegu zake mahali pengi |
| 4 | Tashbihi | Mwenye nguvu kama simba | Nguvu za kiume |
| 1 | Majazi | Spana | Uwezo wa dhakari kufanya kazi anuwai |
| 5 | Chuku | Wavulana warefu futi tisa | Ubabe wa kimaumbile |
| 6 | Jazanda | Fahali kutoka katika ukoo wa Vayokha wanaopendwa na ng'ombe | Ukware |

**Chanzo: Ukokotezi wa Watafiti**

## HITIMISHO

Kulingana na Litosseliti (2010), usemi ni zaidi ya kipashio cha kiisimu, kwani husimba pia imani, itikadi na tajriba za kijamii ambazo huwaongoza wanajamii namna ya kufikiri, kusema, kutenda na hata kutagusana. Lugha inayotumiwa katika majigambo ya Waisukha katika sherehe za miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili* wa *Mayo* husheheni matumizi mbalimbali ya vipashio vya lugha ambavyo husimba tamathali nyingi za usemi na kujenga taswira kadhaa. Mawazo ya Litosseliti yanakaribiana na ya Simala (2012) anayeeleza kuwa utata wa dhana ya mafumbo huongezeka kwa ajili ya istilahi nyingi zinazohusiana na mafumbo kama vile taswira, uhuishi, takriri na jazanda. Kinachorejelewa hapa ni tamathali za usemi ambazo ni semi zinazohusiana na maana za kauli. Wataalamu hawa wanapendekeza kuwa maana katika tamathali za usemi zinahitaji kufasiriwa na kuchunguzwa kwa kina ili kueleweka kwa urahisi kama vile kwa mfano nadharia ya UCHAMAWADI inavyoelezea (Choge, 2018).

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa tamathali za usemi mathalan majazi kama vile 'spana' katika jigambo la 1, tashbihi mfano 'mwenye nguvu kama simba', chuku kwa mfano 'wavulana warefu futi tisa' na jazanda kama vile 'fahali kutoka katika ukoo wa Vayokha wanavyopendwa na ng'ombe wengi' ili kuashiria ukware katika jigambo la 6. Tamathali hizi za usemi zinasheheni sifa mbalimbali za ubabedume katika majigambo ya Waisukha. Sifa za ubabe zilizobainika kupitia kwa tamathali hizi za usemi ni kama vile ukakamavu, uvumilivu, mwanamume kama aliye na mamlaka kuhusu masuala ya mapenzi, ya umiliki wa mali, jasiri, aliye na ukware, shujaa na sifa nyinginezo.

## MAREJELEO


Alembi, E. (2002). *The Construction of Abanyore on Death through Oral Funeral Poetry.* PhD Thesis. Helsinki University Press.

Arege, T. (2002). Mwongozo wa Kilio cha Haki. Nairobi: SAT Publishers.

Chafetz, J. (1974). *Masculine / Feminine or Human?* Itasca, IL: Peacock Publishers.

Choge, S. C. (1997). *Anthroponimu Asilia za Kinandi kwa Mtazamo wa Kisemantiki*. Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa, Chuo Kikuu Cha Moi, Eldoret, Kenya.

Choge, S. C. (2018). *Makala ya Mhadhara wa LEK 925: Kozi ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi (UCHAMAWADI) kwa Wanafunzi wa Uzamifu.* Chuo Kikuu cha Masinde Muliro Cha Sayansi na Teknolojia, Kakamega, Kenya.

Collins, R. (1971). A Conflict Theory of Sexual Stratification. *In Social Problems*.19, 3-21. Doyle, J.A. (1985). *Sex and Gender*. Iowa: CW Brown Publishers.

Fairclough, N. (2002). *The dialectics of discourse. Textus*, 14(2), 3–10.

Gafkosoft, S. (2017). *Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi.* Paneli la Kiswahili. Swa.gafkosoft.com>fasihi-simulizi. Retrieved on 9/9/2018.

Hemingway, E. (1932). *Death in the Afternoon: Treatise on Spanish Bullfighting*. Retrieved on 2/9/2018.

Izugbara, C. O. (2005). "Hypothesis on the Origin of Hegemonic Masculinity" *In Sexuality in African Magazine*. Lagos Africa Regional Sexuality Resource Centre 2(1), 13-14.

Janovsky, A. (2014). The Art of Language. Figure of Speech. Definition, Types and Examples https://study.com/ retrieved on 10/9/2018

Kabaji, E. (2005*). The Construction of Gender Through the Narrative Process of the African Folktale: A Case Study of the Maragolo Folktale*. PhD Thesis, University of South Africa.

Kabaji, E. (2008). *Masculinity and Ritual Violence: A Study of Bullfighting among the Luhyia of Western Kenya.* Pdf retrieved on 17/9/2018.

Kibigo, M. L. (2019). *Ubabedume katika Majigambo ya Miviga ya Shilembe na Mchezasili wa Mayo ya Waisukha Nchini Kenya kwa Mtazamo wa Kisemantiki. (*Tasnifu ya Uzamifu ambayo imewasilishwa kwa

Utahini, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia, Kakamega, Kenya.

Kimani, W. & C. Rocha. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Litosseliti, L. (2010). *Research Methods in Linguistics.* London, New York: Continuum

Matinde, R. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Matinde, R. (2015). *Uchanganuzi wa Ubabedume katika Majigambo (Amabaiko) ya Abakuria.* Tasnifu ya Uzamifu, Haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Laikipia, Nyahururu, Kenya.

Msokile, M. (1992). Misingi ya Hadithi Fupi. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwamanda, J. (2008). Nadharia ya Fasihi, Uchambuzi na Uhakiki. Dar es Salaam: JPD Company and General Supplies Ltd.

Mwita, B. M. (2005). *Dhima ya Ichingaro za Wakuria Kusawiri Taswira ya Mwanamke*. Tasnifu ya Uzamifu. Eldoret: Ndaki ya Moi.

Ruether, R. (1974). *Religion and Sexism.* New York: Simon and Schuster.

Simala, I. K. (2012). *Sexist Overtones in Kiswahili Female Metaphors: A Critical Analysis.* 42nd Annual Conference on African Languages. Ed. Michael R. Marlo et. El pp. 278-290. Someville, MA.

Simala, I. K. (2013). *Makala ya Mhadhara ya Kozi ya Semantiki kwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Mwaka wa Nne*. Kakamega: Ndaki ya Masinde Muliro ya Sayansi na Teknolojia.

Sokoloff, N. (1980). *Between Money and Love*. New York: Praeger.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Van Dijk, T. A. (2000). Critical Discourse Analysis. Retrieved August 3, 2018, from https://www.discourses.org/OldArticles/Critical%20discourse%20analysis.pdf

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Wanjala, S. F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuo na Ndaki.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Wanjala, S. F. (2015). *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu na Mwaka Kogwa.* Tasnifu ya Uzamifu. Nairobi: Ndaki ya Kenyatta.

Wells-Wilbon, R na Holland, S. (2001. December). *Social learning theory and the Influence of male role models on African American children in PROJECT 2000.*

Wodak, R. & M. Meyer (2008). *Critical Discourse Analysis: History, Agenda, Theory and Methodology*. Retrieved June 10, 2019 from https://pdfs.semanticscholar.org

Wodak, R. (Ed) (2013). *Critical Discourse Analysis*. Vol 1. London: Sage.